

# Kilimo hai ni nini?

Kadiri idadi ya watu inavyoongezeka, mbinu za kilimo zimeimarishwa zaidi ili kuongeza mavuno ya mazao na kuhakikisha tunaweza kulisha idadi ya watu inayoongezeka kila mara.

Mbolea na dawa za kuua wadudu hutumika kwenye mazao, na vile vili wanyama na ndege hufugwa vibandani katikaka msongamano wa juu zaidi ili kuongeza uzalishaji wa maziwa na mayai, au kuharakisha muda unaohitajika kwa mnyama kuwa tayari kipelekwa sokoni kuchinjwa. Mbinu mbadala ya kilimo cha kawaida ni kilimo-hai na imependekezwa sana kutokana na uwezo wake wa kukabiliana na shida ya mabadiliko ya hali ya hewa.

## Kilimo Hai

Kilimo-hai kwa sasa kinachukua takriban 1% ya ardhi ya kilimo duniani kote. Kinazingatia uendelevu wa uzalishaji wa mawazo pamoja na kupunguza athari kwa mazingira.

Kilimo-hai hakipaswi kutumia mbolea za kemikali, dawa za kuulia magugu na viuwa wadudu au viungio vya malisho. Kinahitaji mkulima kutumia njia mbadala za asili. Huku husababisha mavuno kidogo, hapokuwa mkulima anaweza kuuza mazao yake kwa bei ya juu.

## Pembejeo

Badala ya mbolea za madini, mbolea za kikaboni au mboji hutumiwa. Hii hurejesha taka na kuboresha muundo wa udongo. Hata hivyo, mboji ina harufu kali na ngumu kutumia shambani kuliko mbolea za kemikali.

Mzunguko wa mazao hutumiwa kupunguza magonjwa ya udongo na kuimarishe muundo wa udongo. Mazao fulani kama vile kunde hutengeneza nitrojeni ardhini kutoka hewani. Badala ya kutumia dawa za kuulia magugu, kupalilia ni mbinu inayopendekezwa ya kilimo-hai.